



Dk. Devon Q. Horton, *Msimamizi*

Bw. Diijon DaCosta, Sr., *Mwenyekiti wa Bodi*  
Bi. Deirdre P. Pierce, *Makamu Mwenyekiti*  
Bi. Anna Hill  
Bi. Whitney McGinniss  
Bi. Allyson Gevertz  
Bi. Vickie B. Turner  
Dk. Joyce Morley

## INAPASWA KUCHAPISWA BILA KUKAWIA

Jumanne Alhamisi, 25 Julai 2024

### Mawasiliano:

Donald Porter, <i>Ed.D.</i>	678-481-4110
Carla Parker	404-734-1717

## **Msimamizi wa DCSD Ateuliwa kwenye Bodi ya Kwanza ya Ushauri wa Usalama wa Shule ya Homeland Security**

*Dkt. Horton anajunga na kundi hili la heshima na wataalamu wa usalama wa kitaifa na viongozi wa elimu*

(STONE MOUNTAIN, GA)— Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) ina fahari kutangaza kuwa Msimamizi Dkt. Devon Q. Horton amechaguliwa kuhudumu katika Bodi Kuu ya Ushauri wa Nje ya Usalama wa Shule iliyoanzishwa na Idara ya Usalama wa Ndani (Department of Homeland Security, DHS). Bodi hii yenye ushawishi mkubwa inajumuisha wataalamu wa usalama wa shule na viongozi wa elimu ambao hutoa maelekezo na mapendeleko muhimu ili kuboresha ulinzi na usalama wa shule za Chekechea hadi gredi ya 12.

Bodi hii ya Ushauri itamshauri Katibu wa Usalama wa Ndani Alejandro N. Mayorkas kupitia Shirika la Usalama wa Miundombinu na Usalama wa Mtandaoni (Cybersecurity and Infrastructure Security Agency, CISA) katika kutekeleza mbinu zinazotegemea ushahidi za usalama wa shule. Mapendeleko ya bodi yatachapishwa katika [SchoolSafety.gov](#), mfumo wa shirikisho unaotoa nyenzo na maelekezo ya usalama wa shule.

“Ninashukuru kuhudumu katika bodi hii ya ushauri na kuchangia katika juhudzi za kitaifa za kuunda mazingira salama ya kujifunzia. Katika ulimwengu wenye matishio yanayobadilika kila mara na ya hali ya juu, ninaamini uzoefu wetu wa pamoja utakuwa wa muhimu katika kusaidia kukuza masuluhisho halisi ambayo yanaboresha ulinzi kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii zetu,” Dkt. Horton alisema.

[Tangazo la wiki hii la DHS](#) linakuja karibu miaka miwili baada ya [Sheria ya Jamii Salama Zaidi Iliyopitishwa na Bunge zote Mbili](#) kupanua Kituo Kikuu cha Shirikisho cha Usalama wa Shule na kuamrishwa uundaji wa bodi yake ya ushauri. Bodii inawakilisha mitazamo mbalimbali kutoka nyanja tofauti, ikiwa pamoja na elimu, usalama wa umma, usalama wa mtandaoni na haki za kiraia.

Orodha kamili ya wajumbe wa bodi hii ya kwanza inapatikana [HAPA](#).

CISA itaalika bodi kwa mukutano wake wa kwanza katika msimu wa Mapukutiko wa 2024.

XXX